

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA KUMI NA TATU**

**27 APRILI, 2022**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA TATU – TAREHE 27 APRILI, 2022

#### I. DUA

#### II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

##### WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

##### WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

## **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

## **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **97. MHESHIMIWA ISSA JUMANNE MTEMVU (KIBAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli utakamilika pamoja na kuhakikisha Kituo hiki kinafanya kazi kama kilivyokusudiwa.

**98. MHESHIMIWA ABEID RAMADHANI IGHONDO (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka Vifaa Tiba katika Hospitali ya Ilongero pamoja na Vituo vya Afya Msange na Mgori Wilayani Singida.

**99. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE (TABORA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itabadilisha mtambo wa kutengeneza hewa ya Naitrojeni Kituo cha Afya Upuge na kuleta mtambo wa hewa ya Oksijeni.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**100. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-



Je, ni lini Serikali itafufua Shule za Msingi za Ufundi Wilayani Hai na kurejesha mfumo wa Wanafunzi kufanya mitihani na kupewa Vyeti.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**101. MHESHIMIWA MWANAKHAMIS KASSIM SAID (MAGOMENI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Wakazi wa Kijiji cha Dunga - Zanzibar.

**WIZARA YA MAJI:**

**102. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati miundombinu ya maji katika Kata za Jimbo la Arumeru Mashariki.

**WIZARA YA KILIMO:**

**103. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP  
MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha Wakala wa kudhibiti Mazao ya Mbogamboga na Matunda nchini.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**104. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA  
(NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya ulinzi kutoka Mtwara – Newala – Masasi hadi Songea kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA  
BIASHARA:**

**105. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, ni kwa nini Serikali imeshindwa kukamilisha ujenzi wa Soko la Kimkakati la Kimataifa la Remagwe.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**106. MHESHIMIWA HASSAN SELEMAN MTENGA (MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni lini Serikali itasaidia Vikundi vya Uvuvi Jimbo la Mtwara Mjini.



**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**107. MHESHIMIWA KHAMIS MBAROUK AMOUR (TUMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Tanzania inapokea Watalii wa aina ngapi kutoka nje na Sekta hii inachangia kiasi gani katika pato la Taifa kwa Mwaka.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**DODOMA  
27 APRILI, 2022**



**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**